**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO CHA KUJADILI TAARIFA ZA ROBO YA TATU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 CHA TAREHE 29/05/2024**

## MAHUDHURIO

### A: WAJUMBE

| S/N | JINA | CHEO | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe Pancras Maliyatabu | -Diwani Kata ya Mtenga | -Mwenyekiti |
| 2. | William Mwakalambile | -Mkurugenzi Mtendaji(W) | -Katibu |
| 3. | Mhe: Stephen Kayogolo | -Diwani kata ya Isale | -Mjumbe |
| 4. | Mhe: Privatus Yolam | -Diwani Kata ya Kala | -Mjumbe |
| 5. | Mhe: Francis Nkoswe | -Diwani Kata ya Ntuchi | -Mjumbe |
| 6. | Mhe: Kudra Ahamad | -Diwani Kata ya Kipundu | -Mjumbe |
| 7. | Mhe: Kakuli Seba | -Diwani Kata ya Kirando | -Mjumbe |
| 8. | Mhe: Vitalis Malipesa | -Diwani Kata ya Korongwe | -Mjumbe |
| 9. | Mhe: Mpemba Evarist | -Diwani Kata ya Nkandasi | -Mjumbe |
| 10. | Mhe George Saninga | -Diwani Kata ya Myula | -Mjumbe |
| 11. | Mhe: Loswiata Sululu | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Wampembe | -Mjumbe |
| 12. | Mhe: Emiliana Kauzeni | -Diwani Viti Maalum Tarafa ya Kate | -Mjumbe |

### WASIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe: Aida Khenani | -Mbunge Jimbo la Nkasi kaskazini | -Kwa Taarifa |
| 2. | Mhe Vicent Mbogo | -Mbunge Jimbo la Nkasi Kusini | -Kwa Taarifa |

### B WATAALAM

| Na | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Dkt John Tlatlaa | Afisa Mifugo (W) |
| 2. | Ndg Valeriana Mwapasi | Afisa Mali asili na Uhifadhi Mazingira(W) |
| 3. | Ndg Mayuma Nzilantuzu | Afisa Usafi na Udhibiti Taka Ngumu(W) |
| 4. | Ndg Dafrosa Mkenda | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 5. | Ndg Nicodemas Hillu | Afisa Ardhi (W) |
| 6. | Ndg Nsubisi Mwakasege | Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W) |
| 7. | Ndg Charles Kisanga | Kaimu Afisa Elimu Msingi(W) |
| 8. | Ndg Alinuntwa Nkundwe | Kaimu Afisa Ugavi na Manunuzi(W) |
| 9. | Ndg Christopher ndinda | Kaimu Afisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji |
| 10. | Ndg Erick Kilimo | Kaimu Mweka Hazina(W) |
| 11. | Ndg Victor Makoba | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 12. | Ndg Steward Vidoga | Kaimu Afisa Mipango na Uratibu(W) |
| 13. | Ndg Salu Makoye | Kaimu Mkaguzi wa Ndani(W) |
| 14. | Ndg Lupakisyo mwakasege | Kaimu Afisa Biashara, Viwanda na Uwekezaji(W) |

15. Ndg Josepha Joseph — Kaimu Mganga Mkuu(W)
16. Ndg Charles Claudio — Kaimu Afisa Mawasiliano
17. Ndg Bakyemba Nicholaus — Kaimu Afisa TEHAMA
18. Eng Gido Monji — Kaimu Mhandisi wa Ujenzi
19. Ndg Didas sadani — Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri
20. Ndg Lucas Mhigi — Mratibu wa TASAF III (W)
21. Ndg Hussen Membe — Kaimu Mthibiti Ubora wa Shule(W)
22. Ndg Richard Katyega — Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu
23. Ndg Rashid Masooud — Kaimu Mtendaji wa mamlaka ya mji mdogo namanyere
24. Ndg Marieta mwanisenga — kaimu afisa utamaduni.

**B SEKRETARIETI**

1. Ndg Patrick Kipesha — Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri
2. Ndg John Mnungwasa — Mhudumu wa Ofisi

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/01/05/2024**
**KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 09.30 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe waliohudhuria na kusisitiza wajumbe kuchangia mawazo kwa kadri ya agenda zilivyoandaliwa na kuwasilishwa mbele yao kwa maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/02/05/2024**
**KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe walithibitisha agenda.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/03/05/2024**
**KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA**

Wajumbe waliupitia muhtasari wa kikao kilichopita ukurasa kwa ukurasa na kufanya marekebisho yaliyojitokeza kisha walikubali muhtasari usainiwe kama kumbukumbu sahihi ya kikao kilichopita.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/04/05/2024**
**YATOKANAYO NA KIKAO KILICHOPITA**

- **Maafisa uvuvi waitwe kwenye kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ili kujadili namna ya ukusanyaji mapato yatokanayo na uvuvi.** Katika utekelezaji ilielezwa kuwa agizo limetekelezwa maafisa uvuvi waliitwa na wamefika, Baaada ya hapo Wajumbe hawakumuona Mkuu wa sekta ya Uvuvi bwana Nova Mlowe na wajumbe walimuhitaji na waliagiza kuwa aitwe katika kikao kijacho
- **Ufuatiliaji ufanyike katika soko la kamwanda-kirando ili kuona mapungufu na mahitaji katika soko hilo ili lifanye kazi kwa ufanisi.** Katika utekelezaji ilielezwa kuwa Kazi ya upimaji, kuandaa ramani ya vibanda imekamilika. Zoezi linalofuata ni kuandaa mikataba ili wananchi watakaopimiwa waweze kujaza na ujenzi uanze mara moja Wajumbe walipokea taarifa na kupongeza kwa kazi nzuri na kushauri michakato iliyobaki iendelee ili wafanyabiashara waanze ujenzi wa vibanda vyao
- **Kikao kazi kifanyike kati ya Maafisa Watendaji wa Kata na Managementi(CMT) ili kuweka mikakati ya ukusanyaji wa mapato** Katika utekelezaji ilielezwa kuwa kikao kazi kilifanyika tarehe 10/05/2023 kilichokutanisha Menejimenti na Watendaji wa kata na mikakati mbalimbali iliwekwa kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato Wajumbe walipokea taarifa na kusisitiza mikakati hiyo isimamiwe ili kuongeza ukusanyaji wa mapato
- **Ufuatiliaji ufanyike kwa mkusanyaji wa mapato kijiji cha kisula ili akabidhi mashine ya kukusanyia mapato POS.** Katika utekelezaji ilielezwa kuwa Ufuatiliaji umefanyika, POS hiyo ilishachukuliwa na amekabidhiwa Mtendaji wa kijiji cha kisula na inaendelea

kukusanya Wajumbe walipokea taarifa na kushauri kuwa wakusanya mapato wanaoidai Halmashauri walipwe fedha zao ili kuwatia moyo katika ukusanyaji.

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/05/05/2024**

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI 2024**

Kaimu Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa Mwezi Machi 2024. Aliwaeleza wajumbe kuwa Katika kipindi cha mwezi Machi 2024 Halmashauri imekusanya mapato ya ndani kutoka vyanzo vyake Jumla ya Tshs. 141,827,434 Hivyo kufanya kiasi kilichokusanywa kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 kuwa Jumla ya Tshs 1,403,508,787 sawa na asilimia 54 ya bajeti ya mwaka 2023/24 ya Tshs 3,133,755,000.00

Aidha Halmashauri kwa mwezi Machi 2024 ilipokea fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kama ifuatavyo: -Mishahara Tshs 21,082,510,000.00, Matumizi mengineyo Tshs 1,465,102,000.00, Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo Tshs 11,994,167,200.00.

Hivyo kuanzia mwezi Julai 2023 hadi Machi 2024 Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs 15,464,722,301 sawa na asilimia 73 ya makisio ya mwaka

Katika kipindi cha mwezi Machi 2024 Halmashauri ilitumia kiasi cha Tshs 279,051,324 kutoka mapato ya ndani. Hivyo kufanya fedha zilizotumika Mwezi Julai 2023 hadi Machi 2024 kuwa Tshs 2,704,408,871.00 sawa na asilimia 23 ya bajeti ya mwaka; Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo.

-Mjumbe alishauri mwezi Agosti 2024 ziwa Tanganyika litakapofunguliwa maafisa uvuvi wapewe POS Mashine ili waweze kukusanya

-Wajumbe walishauri vyanzo vipya vya mapato viibuliwe ili kupandisha mapato ya Halmashauri

-Mjumbe mwingine alishauri udhibiti wa mianya ya kutorosha mizigo uwepo kwani kwa sasa bado mizigo inatoroshwa sana

-Mjumbe mwingine alishauri mapato ya papo kwa papo katika zahanati na vituo vya afya zikusanywe na kuingizwa katika mfumo.

Baada ya majadiliano ya kina Mweka hazina alipokea ushauri na kueleza mikakati mbalimbali iliyowekwa na kuhusu POS Mashine kwenda vituo mbalimbali litatekelezwa Wajumbe walipokea taarifa na kuagiza kama ifuatavyo; *Taarifa iwasilishwe katika kikao kijacho juu ya Ng'ombe waliokamatwa na kutozwa faini kidogo kinyume na taratibu*

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/06/05/2024**

**KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI KWA ROBO YA TATU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

Mwenyekiti wa kamati ya Ukaguzi (W) aliwasilisha taarifa ya kikao cha kamati ya ukaguzi kilichojadili taarifa ya mapato na matumizi kwa robo ya tatu na taarifa ya Mkaguzi wa ndani kwa [illegible] tatu baada ya kujadili [illegible] taarifa hizo kamati iliku[illegible] mapendekezo

mbalimbali ili menejimenti iweze kufanyia kazi kama ifuatavyo; Ndani ya siku kumi na Nne (14) Watumishi ambao hawajarejesha masurufu waandikiwe barua za onyo na warejeshe masurufu kwa mujibu wa sheria , Menejimenti iteuwe mtumishi mmoja kutoka katika kitengo cha Ugavi na Manunuzi kuhakikisha Risiti za mashine za EFD zinafuatiliwa kwa wazabuni mbalimbali wanaotoa huduma Hapa Halmashauri ili kuondokana na changamoto ya hoja ya ukosefu wa Risiti ya EFD katika manunuzi yanayofanyika kutoka kwa wazabuni hao., Menejimenti iandike barua ya kuomba idadi ya wazabuni wanaotekeleza miradi katika taasisi ya TANESCO, RUWASA na TARURA ili waweze kulipa ushuru wa huduma kama sheria inavyotaka. Wajumbe walipokea taarifa na kuagiza maoni ya kamati ya ukaguzi yazingatiwe

## AGENDA NA NKS/DC/FUM/07/05/2024

## KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA IDARA KWA ROBO YA TATU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Idara zifuatazo ziliwasilisha taarifa

### I. IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI

Kaimu Afisa Utawala na Utumishi (W)Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na Idara kwa kipindi cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia aliwasilisha changamoto zinazokabili Idara kama ifuatavyo; Vibali vya ajira mpya na mbadala kutotolewa kwa wakati, upungufu wa vitendea kazi kama magari, pikipiki na kompyuta, upungufu wa nyumba za Watumishi hasa Watendaji Kata na vijiji pamoja na uhaba wa Watumishi hasa Idara ya Afya, Elimu, Utawala, Sheria, Ugavi na Manunuzi, Ardhi, Kilimo na Mifugo.Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Mjumbe alitaka kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya Maafisa Watendaji wa vijiji wanaokunywa pombe muda wa kazi

Afisa Utawala na Utumishi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwaeleza wajumbe kuwa kwa sasa ziara za kustukiza zinafanyika huko vijijini zitawabaini; Wajumbe walipokea taarifa na kuagiza *Idara ya Utawala na Utumishi ifanye ziara ya kuwatembelea watendaji wa vijiji kutokana na watendaji hao kunywa pombe muda wa kazi*

### II. IDARA YA MIPANGO NA URATIBU

Kaimu Afisa Mipango na Uratibu (W) Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia aliwasilisha changamoto zinazokabili Idara kama ifuatavyo; Fedha za Maendeleo zilizokasimiwa katika bajeti kutofika kwa wakati toka Serikali Kuu, hivyo kupelekea miradi ya Maendeleo kutotekelezwa kwa wakati. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

Mjumbe alishauri Idara ya Mipango na Uratibu kutembelea miradi kwa wakati na kutoa ushauri pale panapohitajika. Baada ya hapo Wajumbe waliunga mkono hoja.

## III. KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI

Kaimu Mkaguzi wa ndani(W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na kitengo kwa robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pia aliwasilisha changamoto zinazokabili kitengo kama ifuatavyo; ukosefu wa chombo cha usafiri kwa ajili ya shughuli za ukaguzi wa mara kwa mara wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi mbalimbali ndani ya Halmashauri.

Wajumbe walipokea taarifa na kushauri Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kipewe gari ili kiweze kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa.

## IV. KITENGO CHA SHERIA

Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya shughuli zilizofanyika kwa kipidi cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pia aliainisha changamoto zinazokabili kitengo kuwa ni pamoja na ucheleweshaji wa migogoro ya kisheria kuripotiwa katika kitengo, Kuchelewa kwa maelekezo na miongozo mbalimbali ya kisheria pindi mabadiliko yanapotolewa na Serikali na upungufu wa vitendea kazi. Wajumbe walipokea taarifa na kupongeza kitengo cha Sheria kwa kusimamia kesi mbalimbali. Wajumbe waliunga mkono hoja.

## V. KITENGO CHA TEKNOLOJIA, HABARI NA MAWASILIANO

Kaimu Afisa TEHAMA (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa kwa robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pia alieleza changamoto kama ifuatavyo; uchakavu mkubwa wa vifaa vya kukusanyia mapato (POS Mashine), Ukosefu wa vitendea kazi na ukosefu wa usafiri wa kufika maeneo mbalimbali ya Wilaya kwenda kutatua changamoto za kimfumo. Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia kama ifuatavyo;

-Mjumbe alishauri changamoto za kitengo cha TEHAMA za kutokuwa na vifaa vya kufanyia kazi zitatuliwe ili kitengo kifanye kazi kwa ufanisi

## VI. KITENGO CHA UGAVI NA UNUNUZI

Kaimu Afisa Ugavi na Ununuzi (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa kwa robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia aliwasilisha changamoto zinazo kabili kitengo kama, upungufu wa Watumishi na uhaba wa vitendea kazi. Wajumbe walipokea taarifa na kushauri kitengo

hiki kufanya kazi kwa weredi ili miradi mbalimbali iweze kukamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

## VII. TAARIFA YA TASAF

Mratibu wa TASAF(W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya kazi mbalimbali zilizotekelezwa na TASAF kwa kipindi cha robo ya tatu kwa mwaka

wa fedha 2023/2024 Wajumbe walipokea taarifa na kushauri kuwa Elimu iendelee kutolewa kwa Wananchi ili kuepuka malalamiko mbalimbali yaliyopo

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/08/05/2024**

**KUPOKEA TAARIFA JUU YA UANZISHWAJI, UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA BIASHARA YA HEWA UKAA**

Afisa Usafi wa Mazingira na Udhibiti taka Ngumu (W) aliwasilisha taarifa juu ya mafunzo ya uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa biashara ya hewa ukaa. Aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya wilaya ya Nkasi ni miongoni mwa wilaya iliyozungukwa na misitu mingi ya asili. Misitu hii huchangia kufikia katika kuratibu upunguzaji wa gesi joto zinazosababisha mabadiliko ya tabia za nchi licha ya uwepo wa misitu hiyo Halmashauri ya wilaya ya Nkasi haijanufaika na uwepo wa misitu hiyo ukilinganisha na wilaya zingine zilizo na misitu kama yetu. Aidha kutokana na mafunzo tuliyopata toka wilaya ya Tanganyika biashara ya hewa ukaa inasimamiwa na Halmashauri ikishirikiana na madalali watakaokuwa wameingia mkataba na Halmashauriili. Wajumbe walipokea taarifa na kushauri kuwa jambo hili lifanyike kwa haraka ili mradi huu uanze na fedha zianze kuingia kwa Halmashauri

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/09/05/2024**

**KUPOKEA TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA YA TSHS 121,800,000 KWA AJILI YA UJENZI WA MAJOSHO NA MASHAMBA DARASA YA MALISHO**

Afisa Mifugo (W) aliwasilisha taarifa juu ya mapokezi ya fedha Tshs 121,800,000 kwa ajili ya ujenzi wa majosho na mashamba darasa ya malisho. Aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Wilaya ya nkasi ilipokea barua Kumbu Na CFC.133/307/01/0/72 ya tarehe 17/10/2023 kutoka kwa Katibu Mkuu TAMISEMI ikieleza makatibu Tawala Mikoa kuomba vifungu kutoka wizara ya fedha kwa ajili ya uhamisho wa fedha za maendeleo kutoka Fungu 99 kwenda mafungu ya mikoa mbalimbali. Pamoja na maelezo hayo aliendelea kuwaeleza wajumbe kuwa kiasi cha fedha Tshs 121,800,000 kimepokelewa kutoka katika fungu 99 yaani Wizara ya mifugo na Uvuvi kwa ajili ya ujenzi wa majosho matano (05) kama ifuatavyo; Josho la Paramawe Tshs 23,000,000, josho la Kitosi Tshs 23,000,000, josho la Mtapenda Tshs 23,000,000, josho la Miombo Tshs 23,000,000, josho la Mashete 23,000,000 na shamba darasa la malisho Paramawe na Chatalatila Tshs 6,800,000

Pamoja na mapokezi ya fedha hizo kulikuwa na maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya kuwa kiombwe kibali cha kubadilisha ujenzi wa josho moja kutoka kata ya machete linamie katika kijiji cha Kakoma kilichopo katika kata ya Kipundu chenye Ng'ombe 9,510, hata hivyo kata yenye Ng'ombe wengi ni Mtenga yenye Ng'ombe 16,117. Wajumbe walipokea taarifa na kushauri majosho hayo yajengwe kama ilivyopangwa

**AGENDA NA NKS/DC/FUM/10/05/2024**

**KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA ZIARA YA UKAGUZI WA MIRADI KWA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO**

Afisa Mipango na Uratibu aliwasilisha taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango iliyofanyika kuanzia tarehe 25/05/2024 mpaka tarehe 26/05/2024. Alikieleza kikao kuwa Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ambapo ilitembelea miradi

kama ifuatavyo; ujenzi wa madarasa 2 shule ya sekondari Kate, Ukarabati wa shule kongwe sintali na kala, ujenzi wa choo shule ya Msingi Kacheche, ukarabati wa zahanati kantawa. Wajumbe walipokea taarifa na kupongeza kwa kazi nzuri na kuagiza maagizo yaliachwa katika miradi husika yasimamiwe ili kwenda kutimiza malengo yaliyokusudiwa

## AGENDA NA NKS/DC/FUM/11/05/2024
## TAARIFA YA UWASILISHAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

Kaimu Afisa Mipango na Uratibu (W) aliwasilisha taarifa ya uwasilishaji wa bajeti kwa mwaka 2024/25. Aliwaeleza wajumbe kuwa mkoa wa Rukwa uliwasilisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/2025 mbele ya kamati za kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya tarehe 26/03/2024 katika wasilisho hilo kamati ya bunge ilitoa maagizo ya kutotekelezwa kwa miradi yote ya Ujenzi wa Shule za Mchepuo wa kiingereza kwa kutumia mapato ya ndani. Kwa maelekezo hayo kwa kuwa Halmashauri ilikuwa na mradi wa ujenzi wa shule ya mchepuo wa kiingereza imeshindwa kuanza kwa ujenzi huo. Wajumbe walipokea taarifa na kuagiza suala hili liletwe katika kikao cha kamati ya fedha, Utawala na Mipango ili kuja kutoa maamuzi

## AGENDA NA NKS/DC/FUM/12/05/2024
## MAOMBI YA KUFUTA MADENI YENYE THAMANI YA TSHS 43,336,000 MIKOPO YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W) aliwasilisha ombi la kufuta madeni ya thamani ya Tshs 43,336,000 ikiwa ni mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya wilaya ya Nkasi imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Mikopo hii inatakiwa kurejeshwa kwa muda muafaka kulingana na mkataba.

Pamoja na jitihada kubwa ya kufuatilia kwa kushirikiana na vyombo vya kisheria baadhi ya vikundi vimekuwa vikisumbua kurejesha mikopo hiyo kwa sababu mbalimbali na baadhi ya mikopo imeshindwa kurejeshwa kwa muda muafaka. Mhe Mwenyekiti maombi yanaletwa kwa kamati yako ili iweze kuridhia kufuta madeni katika vikundi vifuatavyo; Isunta Carpenter Group Tshs 450,000, Mwitesi Artist Tshs 6,850,000, Namanyere source of Talent Tshs 5,600,000, Neema ya Mungu Tshs 1,000,000, Skauti Namanyere Tshs 2,800,000, Boda bo[illegible]ndi ya zamani Tshs 1,700,000, Ushirika Korongwe Tshs 2,016,000, Amkeni-Milundikwa Tshs 2,200,000,Shika Hatamu –Kasu Tshs 2,200,000, Ushonaji –Mtenga Tshs 2,200,000, Amani walemavu – kipundu Tshs 2,060,000 na Nkasi intellectual- Isunta Tshs 9,760,000 wajumbe walipokea taarifa na kuagiza kama ifuatavyo;

*Madeni haya yame[illegible]samehewa katika vikundi vyote [illegible] kikundi cha Intelectual kinach[illegible]ngeneza chaki mashine yake ichukuliwe kama kufidia deni na meneja wa kikundi hicho a[illegible]e katika kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.*

## AGENDA NA NKS/DC/FUM/13/05/2024
## MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Mengineyo yaliyojitokeza ni pamoja na

1. Kituo cha afya kasu kinatoa huduma vifungu vyake havijapanuliwa
2. Waheshimiwa madiwani kushiriki katika sherehe za nane nane mwaka huu
3. Vyoo katika shule ya Msingi Kapumpuli vimejaa inatakaiwa kujengwa upya

Baada ya hoja hizo kuibuliwa majibu yalikuwa kama ifuatavyo kuhusu vifungu muda wa kufanya utanuzi wa vifungu ni mwezi wa disemba hivyo tunaomba kuvumilia mpaka muda huo jambo hilo litafanyiwa kazi, kuhusu Waheshimiwa kwenda nane nane litajadiliwa kulingana na bajeti itakavyoruhusu, kuhusu vyoo wananchi wafanye maandalizi ya awali halafu Halamashauri Itachangia pale ambapo panahitajika. Wajumbe walipokea na kuunga mkono hoja.

## AGENDA NA NKS/DC/FUM/14/05/2024
## KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 12:55 mchana.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| WILLIAM, A MWAKALAMBILE | PANCRAS, C MALIYATABU |
| KATIBU | MWENYEKITI |

TAREHE 14/ 06 /2024

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NKASI

THE CHAIRMAN
NKASI DISTRICT COUNCIL